

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BUNGE LA TANZANIA**



MKUTANO WA TANO

YATOKANAYO NA KIKAO CHA TANO

05 NOVEMBA, 2016

MKUTANO WA TANO
YATOKANAYO NA KIKAO CHA TANO - TAREHE 5 NOVEMBA, 2016

I. DUA:

Saa 3.00 asubuhi Mwenyekiti wa Bunge Mhe. Andrew John Chenge alisoma Dua na kuongoza Kikao cha Bunge.

MAKATIBU MEZANI:

1. Ndg. Charles Mloka
2. Ndg. Lawrence Makigi
3. Ndg. Lina Kitosi

II. MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI:

Muswada wa Sheria ya Huduma za Habari wa Mwaka 2016 (*The Media Service Bill, 2016*):

Uchangiaji wa Muswada huu uliendelea kama ifuatavyo:-

- | | | |
|---|---|---------|
| 1. Mhe. Hawa Abdulrahman Ghasia, | - | CCM |
| 2. Mhe. Janeth Zebedayo Mbene | - | CCM |
| 3. Mhe. Ester Michael Mmasi | - | CCM |
| 4. Mhe. Tundu Antiphas Lissu | - | CHADEMA |
| 5. Mhe. Amina Saleh Mollel | - | CCM |
| 6. Mhe. Khatib Said Haji | - | CUF |
| 7. Mhe. Devotha Mathew Minja | - | CHADEMA |
| 8. Mhe. Omar Ally King | - | CCM |
| 9. Mhe. Saada Mkuya Salum | - | CCM |
| 10. Mhe. Zainab Matitu Vullu | - | CCM |
| 11. Mhe. Ridhiwani Jakaya Kikwete | - | CCM |
| 12. Mhe. Januari Yusuf Makamba | - | CCM |
| 13. Mhe. Dkt. Harrison George Mwakyembe | - | CCM |
| 14. Mhe. Dkt. Abdallah Possi | - | CCM |

| | | |
|--|---|-----|
| 15. Mhe. Annastazia James Wambura | - | CCM |
| 16. Mhe. Nape Moses Nnauye (Alihitimisha Hoja) | - | CCM |

III. MWONGOZO WA SPIKA

1. Mhe. John John Mnyika aliomba Mwongozo kwa kutumia Kanuni ya 58(1) na Kanuni ya 88(2) akirejea maelekezo ya Mhe. Mwenyekiti aliyoyatoa siku ya Ijumaa kuhusu kuendelea kufanya tafakari ya Muswada huu ili waweze kutumia fursa hiyo kuwasilisha majedwali ya marekebisho.

Alieleza pia kuwa Wabunge mbalimbali waliwasilisha Majedwali yao kwa Katibu lakini Majedwali hayo hayajaingia Bungeni. Hivyo, alitaka Mwongozo ili Mwenyekiti ajibu kwa nini majedwali mengine yasiingie sasa kabla ya kuingia kwenye Kamati ya Bunge Zima.

Mheshimiwa Mwenyekiti alitoa Mwongozo kwamba, kwa utendaji bora wa Shughuli za Bunge tayari alielekeza kwamba Marekebisho ya Majedwali yanatakiwa kuwasilishwa mapema ili yaweze kuifikia Serikali pamoja na Kanuni kuweka wazi kwamba Majedwali ya Marekebisho yanatakiwa kuletwa wakati wowote haina maana kwamba kusiwe na utaratibu wa kupata Majedwali ya Marekebisho mapema.

IV. KAMATI YA BUNGE ZIMA:

Bunge liliingia katika hatua ya Kamati ya Bunge Zima kupitia Ibara kwa Ibara Muswada wa Huduma za Habari:-

V. BUNGE KURUDIA:

Baada ya Shughuli za Kamati ya Bunge Zima kukamilika, Bunge lilirudia ambapo Mwenyekiti alimwita mtoa Hoja kutoa taarifa ya shughuli zilizofanyika katika Kamati ya Bunge Zima. Mwenyekiti alilihoji Bunge na kupitisha Muswada wa Sheria ya Huduma za Habari wa Mwaka 2016 (*The Media Services Bill, 2016*).

VI. MUSWADA KUSOMWA MARA YA TATU:

Muswada ulisomwa kwa Mara ya Tatu. Mheshimiwa Mweyekiti alitangaza kwamba Muswada huo wa Sheria sasa umepitishwa Rasmi na Bunge na hivyo utapelekewa kwa Mheshimiwa Rais kwa ajili ya hatua ya kusainiwa kabla ya kuwa Sheria kamili.

VII. KUAHIRISHA BUNGE:

Saa 8.40 Mwenyekiti aliahirisha Shughuli za Bunge hadi tarehe 07/11/2016 saa 3.00 Asubuhi.

DODOMA
05 NOVEMBA, 2016

DKT. T. D. KASHILILAH
KATIBU WA BUNGE